



EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA

MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA UJENZI WA AWALI KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) - KUMBUKUMBU NA. 612 503

Kampuni ya Mafuta na Gesi ya TOTAL East Africa Midstream B.V., inakaribisha wazabuni wenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kufanya shughuli za Ujenzi wa Awali nchini Tanzania kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unajumuisha Uhandisi, ujenzi, uendeshaji na usimamiaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukuwa chini ya ardhi na lenye mfumo wa kutunza joto litakalopita Uganda na Tanzania likiwa na mfumo wa umeme wa kufuatilia mwenendo wa joto, miundombinu husika ya juu ya ardhi na kituo cha Kuhifadhi Mafuta Pembezoni mwa Bahari kilicho eneo la Chongoleani, karibu na Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

MAELEZO MAFUPI YA KAZI

Shughuli za Ujenzi wa Awali zitafanyika katika maeneo mbalimbali ya ujenzi katika mikoa ya KAGERA, GEITA, TABORA, SINGIDA, DODOMA, MANYARA, TANGA na itajumuisha shughuli zifuatazo;

- Maandalizi ya eneo** (Usafishaji, usawazishaji, urudishaji wa udongo, utengenezaji mifereji, uzio, n.k.) kwa Kambi kuu & Maeneo ya Kutunzia Mabomba (kila moja likiwa na ukubwa wa mita 300 kwa 500); Eneo la Ufunikaji wa bomba ili liweze kutunza joto lenye ukubwa wa mita 500 kwa 800; na Kambi za kudumu (Vituo vya kuongeza msukumo wa Mafuta vyenye ukubwa wa mita 300 kwa 400 kila kimoja na Vituo vya Kupunguza Msukumo wa Mafuta vyenye ukubwa wa mita 200 kwa 200 kila kimoja na Kituo cha Kuhifadhi Mafuta pembezoni mwa bahari chenye ukubwa wa mita 500 kwa 1300.
- Ujenzi wa barabara wezeshi za kuelekea maeneo ya Mradi** Barabara wezeshi za muda mfupi, barabara wezeshi za muda mrefu, uboreshaji na utunzaji wa barabara zilizopo kwa urefu wa kilomita zipatazo 100 ili kufikia Kambi Kuu na Maeneo ya Kutunzia Mabomba pamoja na Kambi za Muda Mrefu. Barabara wezeshi zote ni za "changarawe" zilizosaniwa kwa "Viwango vya Jumla kwa ajili ya Barabara Wezeshi na Ujenzi wa Jumla wa Eneo Husika la Mradi" vya mwaka 2000, vilivyochapishwa

na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Kazi na mahususi kwa magari yenye semi-trela WB20 yenye urefu wa mita 22.4 na upana wa mita 2.6 kulingana na viwango vya AASHTO. Uboreshaji na utunzaji wa barabara zilizopo na barabara wezeshi za muda mrefu unatakiwa kukidhi viwango vya barabara vya Tanzania daraja DC6; Barabara wezeshi za muda mfupi zinatakiwa kukidhi viwango vya barabara vya Tanzania daraja DC7.

Shughuli hizi za ujenzi zinaambatana na shughuli zingine ambazo ni muhimu katika shughuli za ujenzi wa Awali, kama: Utawala, Usimamizi wa Mradi, uhifadhi kumbukumbu na Uratibu; Uhandisi wa uwandani; shughuli za ugavi na usambazaji wa vitaa.

Kambi kuu na Maeneo ya Kuhifadhi Mabomba yatakuwa katika wilaya zifuatazo: Missenyi, Muleba, Chato, Bukombe, Nzega, Igunga, Singida Vijijini, Kondoa, Kiteto, Kilindi, Halmashauri ya Mji wa Handeni na Muheza.

Kambi za muda mrefu zitakuwa katika wilaya zifuatazo: Muleba, Mbogwe, Igunga, Singida vijijini, Kiteto, Handeni na Tanga.

VIGEZO MUHIMU

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na:

- Ushahidi wa usajili nchini Tanzania kwa shughuli tajwa hapo juu;
- Uzoefu katika shughuli za ujenzi nchini Tanzania: uandaaji wa eneo, kazi za juu ya ardhi (usafishaji, ufukiaji, usawazishaji n.k.), utengenezaji mitaro na barabara;
- Uthibitisho kwa kampuni ina uwezo wa kufanya shughuli hizi katika moja ya maeneo tajwa au zaidi **kwa shughuli za uandaaji wa eneo au ujenzi wa barabara wezeshi**.
- Ushahidi wa kuwa na zana mahususi – vitaa, mfumo na rasimali watu wenye uwezo;
- Ushahidi wa sera mahususi za Ubora na Afya, Usalama na Mazingira (HSE and Quality Policy)

Makampuni yenye nia, vigezo muhimu na yenye uwezo wa kutoa huduma tajwa hapo juu za uandaaji wa eneo na/au ujenzi wa barabara wezeshi, zinatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: contractor-info@eacop-proc.com hadi kufikia saa 11:00 jioni **Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 25 Novemba 2020**.

Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).